Majibu

KUSOMA (QR 2- Ukurasa wa 63)

7. Kusoma kwa kina

i. Novela

Jitathmini 7.1 (ukurasa wa 43)

1. Novela ni utungo wa fasihi andishi wenye urefu wa wastani unaosimulia visa na matukio mbalimbali kuhusu maisha ya wahusika katika jamii.
2. Novela huwa na matukio mengi ikilinganishwa na hadithi fupi.
   Huwa ndefu kushinda hadithi fupi.
   Huwa na wahusika wengi kuliko hadithi fupi.
   Huweza kugawanywa katika sura mbalimbali kinyume na hadithi fupi isiyogawanywa.
3. (a) Amani, Mwalimu mkuu
   (b) Amani alishinda katika shindano la kuandika insha kutokana na juhudi na umakinifu wake.

4. Fanya zoezi hili ukiwa peke yako.

5 (a). Novela hulenga kutoa mafunzo kuhusu maadili fulani.

(b) Baadhi ya wasomaji husoma novela kupitisha muda.

(c) Msomaji wa novela huongeza hazina ya msamiati wake.

(d) Novela hutoa mafunzo kuhusu maisha halisi na hali zinazoikabili jamii fulani.

6. Fanya zoezi hili na mwenzako, mzazi au mlezi wako.

7. Kuwepo kwa uhusiano maalumu wa kiutani kati ya wanaohusika.

8. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama kisha ufanye mazoezi uliyopewa.

9. Zingatia maagizo uliyopewa kufanya zoezi hili.

a. Maudhui na dhamira katika novela

Jitathmini 7.2 (ukurasa wa 43-44)

1. Unaweza kurejelea ulipoandika kwenye shajara yako kujikumbusha novela hiyo ilihusu nini.

2. (a) Hakiki majibu yako kwa kurejelea sehemu ya **Kumbuka** katika ukurasa wa 44.

(b) Hakiki majibu yako kwa kurejelea sehemu ya **Kumbuka** katika ukurasa wa 44.

3. (a) Wizi wa magodoro uliofanywa na mmojawapo wa walinzi aliyeaminiwa sana na hatua za kuimarisha usalama shuleni kama vile ua wenye nyaya za stima na kamera za siri kuwekwa.

(b).

- Usaliti – wizi wa magodoro unafanywa na mlinzi aliyeaminiwa sana.
- Kutowajibika – badala ya mlinzi kulinda usalama wa wanafunzi, anahusika katika wizi wa magodoro.
- Kuwajibika – Bi. Amina anafanya awezalo kuimarisha usalama shuleni.
- Elimu – wanafunzi wamo darasani kengele inapokirizwa.

4.

- Kuonyesha uwajibikaji wa mwalimu mkuu.
- Kuonyesha jinsi watu wanaoaminika katika jamii wanavyowasaliti wengine.
- Kuonyesha umuhimu wa kuimarisha usalama shuleni.

5. (a) Unaweza kuandika kwenye daftari, shajara yako au kwenye kifaa cha kidijitali na uwawasilishie wenzako uchambuzi huo.

6. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama kisha ufanye mazoezi uliyopewa.

7. Rejelea novela uliyoisoma ili uandike dhamira ya mwandishi.

8. Unaweza kuandika kwenye daftari, shajara yako au kwenye kifaa cha kidijitali na uwawasilishie wenzako uchambuzi huo.

9. Fanya zoezi hili ukiwa na mzazi au mlezi wako kisha utambue maudhui na dhamira.

b. Mandhari na ploti katika novela
Jitathmini 7.3 (ukurasa wa 44-45)

1. (a) Mandhari ya nyumbani, shuleni, hospitalini, sokoni, au mandhari ya usiku na mchana.
(b) Ploti inajumuisha: Mwanzo (utangulizi), mzozo/ mgogoro (matatizo yanapoanza), kilele (sehemu ngumu zaidi ya mgogoro) na suluhisho/ utatuzi.

2. (a) Mandhari ni mahali, wakati au mazingira (hali ya kijamii) ambamo matukio ya kazi ya fasihi hutokea.
(b) Ploti ni mtiririko na mpangilio wa matukio ambayo yanajenga hadithi kuanzia mwanzo hadi mwisho (utatuzi).

3 (a) Novela inamwelimisha msomaji kuwa mwangalifu kuhusiana na suala la ulanguzi wa binadamu
(b)

Mandhari ya mahali – Kijiji cha kijani, nje ya nyumba yao, barabarani na shuleni.
Mandhari ya wakati – Jioni/ usiku, siku hiyo, siku iliyofuata, miezi kadhaa iliyopita.
Mandhari ya hali – Umaskini, matumaini, wasiwasi na kutafakuri na ushirikiano.

(c)

- Kujenga na kukuza maudhui kama vile umaskini na ushirikiano.
- Kuendeleza ploti au mtiririko wa hadithi.
- Kusawiri na kubainisha tabia za wahusika, kwa mfano, Asha ni mwenye mawazo tele.
- Kujenga hisa kama vile, hisia ya wasiwasi na tahadhari miongoni mwa vijana baada ya mawaidha ya mwalimu.

4 (a)

- Asha kuwa mwenye mawazo mengi na mwenye kukata tamaa kutokana na umaskini wa familia yao na ukosefu wa ajira baada ya kuhitimu shule katika kijiji cha kijani.
- Bwana Kenga anawatolea vijana ahadi za ulaghai zinazowavutia Asha na vijana wenzake wakiamini kuwa ni mwanzo wa maisha mapya.
- Mwalimu Bi. Rehema anashuku nia ya Bwana Kenga kutokana na ufahamu wake wa ulanguzi wa binadamu na kuitisha mkutano shuleni na kuwaonya vijana dhidi ya kukubadili ahadi hizo.
- Maneno ya Bi. Rehema yanambadilisha Asha na vijana wenzake mawazo.
- Viongozi wa kijiji wanawasiliana na maafisa wa usalama ambao wanafanya uchunguzi na kubaini kuwa Bwana Kenga alikuwa mlanguzi wa binadamu. Kisha Bwana Kenga anakamatwa na polisi.
- Asha anajifunza umuhimu wa kuwa mwangalifu na kutafuta ushauri kabla ya kufanya maamuzi makubwa maishani.
- Kijiji kizima kinachukua hatua ya kuanza kuelimisha vijana mara kwa mara kuhusu hatari za ulanguzi wa binadamu ili kuzuia ulaghai kama huo katika siku zijazo.

(b)

- Ploti imesaidia kujenga kisa mgogoro wa novela hii kuanzia Asha kusongwa na mawazo hadi Bwana Kenga kutuhumiwa kuwa mlanguzi wa binadamu.
- Ploti katika novela hii imesaidia kutatua mgogoro wa hadithi. Kijiji kizima cha Kijani kinaanza kuwaelimisha vijana kuhusu hatari za ulanguzi wa binadamu baada ya uchunguzi kubaini kuwa Bwana Kenga ni mlanguzi mkuu wa binadamu.

5(a)

- Mandhari ya mahali – Kijiji cha Kijani, nje ya nyumba yao, barabarani na shuleni. Mandhari haya yanamwezesha msomaji kutambua matukio yanatendekea wapi.
- Mandhari ya wakati – Jioni/ usiku, siku hiyo, siku iliyofuata, miezi kadhaa iliyopita. Mandhari haya ya wakati yanamsaidia msomaji kutambua matukio ya sehemu hii ya novela yanatokea wakati gani.
- Mandhari ya hali – Umaskini, matumaini, wasiwasi na kutafakuri na ushirikiano. Mandhari haya ya hali humsaidia msomaji kuelewa hali ya kimawazo au kimaisha ya wahusika katika sehemu hii ya novela.

6. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama kisha ufanye mazoezi uliyopewa.

1. Fanya zoezi hili na mzazi au mlezi wako.

c. Wahusika katika novela

Jitathmini 7.4 (ukurasa wa 45-46)

1. Hakiki majibu yako kwa kurejelea sehemu ya **Kumbuka** katika ukurasa wa 46.

2. (a) Binti, Gresi, Mwalimu Njoga

(b)

- Binti – mvumilivu kwa vile anavumilia ubaguzi anaoupitia na mwishowe anaibuka mshindi.
- Gresi ni mbaguzi kwa vile anambagua Binti.
- Bwana Njoga ni mshauri mwema kwa vile anamshauri Binti.

(c)

- Binti ni mwanafunzi wa Mwalimu Njoga na ni rafiki yake Gresi.
- Mwalimu Njoga ni mwalimu wake Binti na Gresi.
- Gresi ni rafiki yake Binti na ni mwanafunzi wa Mwalimu Njoga.

3. (a) Hatufai kubagua watu kwa misingi yoyote.

(b) Tunafaa kuwatia watu moyo bila kuwabagua kwa njia yoyote ile.

(c) Tusiache maneno ya watu yatufanye tufe moyo na kukata tamaa maishani.

4. Igiza wahusika hao kwa kuangazia matendo na maneno yao.

5. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama kisha ufanye mazoezi uliyopewa.

6. Unaweza kusoma maktabani au kwenye mtandao salama kisha uchambue wahusika na sifa zao.

7. Fanya zoezi hili ukiwa na mzazi au mlezi wako kisha mjadiliane kuhusu wahusika wake.

d. Mbinu za lugha katika novela

Jitathmini 7.5 (ukurasa wa 46-47)

2 (a)

- Hupunguza ukinaifu unaotokana na matumizi ya lugha kavu.
- Humchorea msomaji picha akilini ambayo inamwezesha kuelewa ujumbe unaopitishwa.
- Hutumika kuifanya kazi ya fasihi iwe ya kuvutia na kusisimua kwa msomaji
- Huyafanya maelezo yawe bayana na hivyo kueleweka kwa urahisi.
- Hutumika kuimarisha ubunifu wa mwandishi.
- Hutumika kuchochea hisia za msomaji wa kazi bunilizi.
- Hutumika kumburudisha msomaji.

(b) Mbinu za lugha ni matumizi ya maneno kwa njia wa usanii. Mifano ya mbinu za lugha ni kama vile sitiari, takriri, majazi, tashbihi, sitiari, nahau na methali.

(c)

- Tashbihi- tia bidii kama mchwa.
- Methali- mtaka cha mvunguni sharti ainame, kutangulia si kufika
- Nahau- piga hatua, ng'oa nanga

(d)

- Kutumika kuifanya kazi ya fasihi iwe ya kuvutia na kusisimua kwa msomaji.
- Kuyafanya maelezo yawe bayana na hivyo kueleweka kwa urahisi.
- Kuimarisha ubunifu wa mwandishi.
- Kuchochea hisia za msomaji wa kazi bunilizi.
- Kumburudisha msomaji.

3. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama kisha ufanye mazoezi uliyopewa.

4. Fanya zoezi hili na mzazi ai mlezi wako.

ii. Tamthilia

Jitathmini 7.6 (ukurasa wa 47-48)

1. Tamthilia ni utungo wa fasihi andishi unaoigizwa jukwaani mbele ya hadhira au watazamaji.
2.
    - Wahusika
    - Vitendo
    - Mazungumzo
    - Jukwaa
    - Ujumbe
    - Mandhari

4. (a) Mwalimu Mkuu, Juma, Asha

(b) Shuleni, asubuhi

(c) Mwalimu Mkuu anawasisitizia Juma na Asha umuhimu wa elimu na kuwahimiza wafike shuleni mapema.

(d) Hakiki hoja zako kwa kurejelea sehemu ya **Kumbuka** katika ukurasa wa 47-48.

(e) Kuinamisha kichwa, kutikisa kichwa

5. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama kisha ufanye mazoezi uliyopewa.

7 (a) Kuelimisha jamii - Tamthilia hutumika kutoa funzo chanya kwa jamii.

(b) Kuwaburudisha watazamaji – baadhi ya wasomaji husoma tamthilia ili kupitisha muda.

(c) Kukuza maadili – Tamthilia huelimisha jamii kuhusu maadili fulani.

(d) Kukuza lugha na mawasiliano – wasomaji wa tamthilia hukuza msamiati na kuimarisha lugha.

9. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama kisha ufanye mazoezi uliyopewa.

10. Fanya zoezi hili na mzazi au mlezi wako.

a. Maudhui na dhamira katika tamthilia
Jitathmini 7.7 (ukurasa wa 48-49)

1. Unaweza kurejelea ulipoandika kwenye shajara yako kujikumbusha mambo muhimu katika tamthilia hiyo.
2. (a) Hakiki majibu yako kwa kurejelea sehemu ya **Kumbuka** katika ukurasa wa 44.
(b) Hakiki majibu yako kwa kurejelea sehemu ya **Kumbuka** katika ukurasa wa 44.
3. Soma kwa kuzingatia matamshi bora na viakifishi ifaavyo.
(a) usalama nyumbani, usalama unapotumia vifaa vya kidijitali
(b) Kutowajibika – Joni anaweka chaja kwenye soketi na anaacha nyaya zake zizagae sakafuni eneo la kupita.
Kuwajibika – Baba huwaambia kuwa hawafai kutumia simu wakati inachaji.
4. Kuonyesha jinsi usalama nyumbani unafaa kuimarishwa.
5. (a) Unaweza kuandika kwenye daftari, shajara yako au kwenye kifaa cha kidijitali na uwawasilishie wenzako uchambuzi huo.
6. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama kisha ufanye mazoezi uliyopewa.
7. Rejelea tamthilia uliyoisoma ili uandike dhamira ya mwandishi.
8. Unaweza kuandika kwenye daftari, shajara yako au kwenye kifaa cha kidijitali na uwawasilishie wenzako uchambuzi huo.
9. Fanya zoezi hili ukiwa na mzazi au mlezi wako kisha utambue maudhui na dhamira.

a. Mandhari na ploti katika tamthilia
Jitathmini 7.8 (ukurasa wa 49)

1 (a) Mfano wa jibu: Mandhari ya sebuleni mwa wahusika, ikulu, mahakamani, au wakati wa jioni/asubuhi na mandhari ya hali kama vile hofu, masikitiko, umaskini n.k.
(b) Inasaidia kupanga matendo na mazungumzo ya wahusika kwa mtiririko unaoeleweka, kukuza mgogoro, na kumvuta msomaji au mtazamaji kufuatilia mchezo hadi mwisho, kujenga ujumbe, kutoa funzo, kufichua wahusika na kuibua mandhari mbalimbali.
2. (a) Ni mazingira, mahali, au majira/ muda ambapo wahusika wa tamthilia wanatendea matendo yao.
(b) Ni muundo na mtiririko wa matukio yaliyopangwa kwa kimantiki ili kuonyesha mwanzo, kukua, na kusuluhishwa kwa mgogoro katika tamthilia.
3 (a) Matumizi ya teknolojia na tahadhari dhidi ya uhalifu/utapeli wa mtandaoni.

(b)
- Mandhari ya mahali – Nyumbani
- Mandhari ya wakati – Jioni
- Mandhari ya hali – Wasiwasi, utapeli

(c)
- Kusawiri wahusika kama vile Sara, Daudi na mama.
- Kuibua matendo ya wahusika kwa mfano, Sara ameketi akibofya simu huku Daudi akisoma.
- Kuibua hisia za wahusika kama vile Sara ana wasiwasi.
- Kujenga maudhui kama vile teknolojia.
- Kujenga mbinu za lugha kwa mfano taswira.

4 (a)
- Mama anawakuta Sara na Daudi wakitumia vifaa vyao vya kidijitali jioni nyumbani na kuwatahadharisha kuhusu uhalifu wa mtandaoni.
- Sara anauliza uhalifu huo ni nini na baada ya kuelezwa anashtuka na kukiri kuwa amepokea ujumbe wa kitapeli unaoomba nambari yake ya siri ya simu.
- Daudi na mama wanathibitisha kuwa huo ni utapeli na mama anatoa kanuni kali za usalama.
- Sara na Daudi wanaahidi kuwa waangalifu na wote wanakubaliana kuwa teknolojia ni nzuri lakini inahitaji uangalifu.

(b)
- Kujenga mtiririko wa ujumbe.
- Kukuza mgogoro
- Kutoa mafunzo kwa wasomaji.
- Kutambulisha wahusika.
- Kuibua maudhui.
- Kuibua tamathali za usemi.

5. Andika maelezo hayo daftarini au kwenye shajara yako.
6. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama kisha ufanye mazoezi uliyopewa.
7. Fanya zoezi hili na mzazi au mlezi wako.

b. Wahusika katika tamthilia

Jitathmini 7.9 (ukurasa wa 49-50)

1. (a) Hakiki majibu yako kwa kurejelea sehemu ya **Kumbuka** katika ukurasa wa 50.

(b) Jibu kulingana na tamthilia ambayo umewahi kuisoma.

2. (a) Boni, Koki, Baba

(b)
- Boni ni mnyenyekevu kwa vile anaomba msamaha kwa Koki anapomkosea.
- Koki ni msamehevu kwa vile anamsemehe Boni
- Baba ni mwenye busara na mshauri mwema kwa vile anampa Koki ushauri unaomsaidia kudhibiti hisia zake.

(c) Andika kwenye daftari au kwenye kifaa cha kidijitali.

(d) Boni na Koki ni ndugu, Baba ni mzazi wa Boni na Koki

3.
- Ni vyema kushauri na kupatanisha watu wanaogombana.

- Hatufai kukasirika haraka, tunafaa kujua jinsi ya kudhibiti hisia na pia tunafaa kuwasamehe wanaotukosea.
- Tunafaa kuomba msamaha tunapokosa.

4. Igiza wahusika hao kwa kuangazia matendo na maneno yao.
5. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama kisha ufanye mazoezi uliyopewa.
6. Unaweza kusoma maktabani au kwenye mtandao salama kisha uchambue wahusika na sifa zao.

d. Mbinu za lugha katika tamthilia
Jitathmini 7.10 (ukurasa wa 50-51)

1. Tasfida, uradidi, taswira, methali, tashbihi.

2 (a).

- Hupunguza ukinaifu unaotokana na matumizi ya lugha kavu.
- Humchorea msomaji picha akilini ambayo inamwezesha kuelewa ujumbe unaopitishwa.
- Hutumika kuifanya kazi ya fasihi iwe ya kuvutia na kusisimua kwa msomaji
- Huyafanya maelezo yawe bayana na hivyo kueleweka kwa urahisi.
- Hutumika kuimarisha ubunifu wa mwandishi.
- Hutumika kuchochea hisia za msomaji wa kazi bunilizi.
- Hutumika kumburudisha msomaji.

(b) Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama kisha ufanye zoezi ulilopewa.

(c) Fanya zoezi hili na mzazi au mlezi wako.

iii. Ushairi

Jitathmini 7.11 (ukurasa wa 51-52)

1. Shairi ni utungo wa fasihi andishi unaotumia lugha ya kisanaa yenye mpangilio maalum wa mishororo, beti, vina na mizani ili kuwasilishaujumbe fulani kwa jamii.

4 (a) Umuhimu wa bidii, elimu na uvumilivu katika jamii.

(b)

- Utungo huu una beti tatu.
- Kila ubeti una mishororo minne.

(c) Matumizi ya sitiari, tanakali za sauti.

(d) Lugha ya picha humjengea msomaji picha akilini na kusaidia kuelewa ujumbe unaowasilishwa.

5. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama kisha ufanye zoezi ulilopewa.

6. Hakiki hoja zako kwa kurejelea sehemu ya **Kumbuka** katika ukurasa wa 52.

8 (a)

- Shairi limegawika katika beti ilhali tanzu nyingine za fasihi zimegawika katika aya.
- Shairi huwa na nafsineni na nafsinenewa ilihali tanzu nyingine zina msimulizi na wahusika.
- Beti za shairi hugawika katika mishororo na vina ilhali tanzu nyingine hazina sifa hii.

9. Fanya zoezi hili na wenzako.

10. Shairi linahimiza kuhusu maadili ya bidii, uvumilivu na umuhimu wa elimu.

a. Maudhui na dhamira katika ushairi

Jitathmini 7.12 (ukurasa wa 52)

1. Unaweza kurejelea ulipoandika kwenye shajara yako kujikumbusha mambo muhimu katika mashairi uliyowahi kusoma.
2. (a) Hakiki majibu yako kwa kurejelea sehemu ya **Kiangaza** katika ukurasa wa 52.
(b) Dhamira katika shairi ni lengo la shairi kama vile kuonya, kuhamasisha, kuelimisha, kuburudisha, kukosoa, kukanya, miongoni mwa nyingine.
(c) Idadi ya beti, idadi ya mishororo katika ubeti, idadi ya mizani katika mshororo, idadi ya vipande katika mshororo, mpangilio wa vina na iwapo shairi lina kibwagizo au la.
3. (a) usalama barabarani, njia za kuhakikisha usalama barabarani
(b) Kuwajibika – nafsineni anaambia watu wajukumike kuhakikisha usalama barabarani
(c) Shairi hili lina beti tano, kila ubeti una mizhororo minne, kila mshororo una vipande viwili, kila mshororo una mizani 16, vina vya kati na mwisho vinafanana, shairi lina kibwagizo ambacho ni ‘Usalama wa njiani, sote tujukumikeni’
4. Kuonyesha jinsi usalama barabarani unafaa kuimarishwa.
5. Unaweza kuandika kwenye daftari, shajara yako au kwenye kifaa cha kidijitali na uwawasilishie wenzako uchambuzi huo.
6. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama kisha ufanye mazoezi uliyopewa.
7. Rejelea mashairi uliyoyasoma ili uandike dhamira ya mwandishi.
8. Unaweza kuandika kwenye daftari, shajara yako au kwenye kifaa cha kidijitali na uwawasilishie wenzako uchambuzi huo.

b. Mandhari na muundo katika ushairi

Jitathmini 7.13 (ukurasa wa 53)

1.(a) Kwa mfano: Yana mandhari ya huzuni, umaskini, hofu, uharibifu wa mazingira, au mandhari ya kijamii yenye matatizo.
(b) Vinahusu umbo la nje la shairi linaloonekana kwa macho kama vile beti, mishororo, vipande, vina, mizani, na kibwagizo.
2. (a) Ni mazingira au hali ya kihemko/ kijamii na wakati unaozungumziwa katika utunzi na uwasilishaji wa shairi (kama vile hali ya simanzi au furaha).
2. (b) Unahusisha mpangilio maalumu wa maneno na mistari, ikiwemo idadi ya beti, mistari katika kila ubeti, silabi (mizani), na urari wa sauti (vina).
3 (a) Matatizo na changamoto mbalimbali zinazoikabili jamii kwa sasa.
(b)

- Mandhari ya mahali – Dunia, hospitali
- Mandhari ya hali – Chuki, umaskini, mashaka, dhiki na njaa.

4 (a) Shairi hili lina beti 4
(b) Kila ubeti una mishororo 4
(c) Kila mshororo una vipande 2
5.

- Kusaidia msomaji kuelewa ujumbe na hisia za mtunzi.
- Kutoa funzo au mwamko wa mabadiliko.
- Kusawiri masuala/ maudhui kama vile vifo.
- Kujenga ploti.
- Kuibua tamathali za usemi kama vile taswira.

6. Andika daftarini au katika shajara yako.
7. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama kisha ufanye mazoezi uliyopewa.
8. Fanya zoezi hili na mzazi au mlezi wako.

c. Wahusika katika ushairi

Jitathmini 7.14 (ukurasa wa 53-54)

1. Jibu kulingana na mashairi ambayo umewahi kuyasoma.
2. (a) Nafsineni ni tabibu, nafsinenewa ni Susi
(b)

- Tabibu ni mshauri mwema kwa vile anampa Susi ushauri wa kukabili msongo wa mawazo
- Susi ni msikivu kwa vile anamsikiliza tabibu akimpa ushauri

(c) Andika kwenye daftari au kwenye kifaa cha kidijitali.
(d) Tabibu ni mshauri wa Susi.
3. Ni vyema kutafuta namna zote za kukabiliana na msongo wa mawazo.
4. Igizeni wahusika hao kwa kuangazia matendo na maneno yao.
5. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama kisha ufanye mazoezi uliyopewa.
6. Unaweza kumsomea kitabuni au kwenye mtandao salama kisha mjadiliane kuhusu wahusika wake.

c. Mbinu za lugha katika ushairi

Jitathmini 7.15 (ukurasa wa 54)

1.

- Hutumika kujenga picha akilini mwa msomaji.
- Hutumika kuwasilisha ujumbe mzito kwa maneno machache.
- Humvutia msomaji na kumburudisha.
- Hutilia mkazo ujumbe unaopitishwa.
- Hutumika kuipamba lugha na kuitofautisha na lugha ya kawaida.

2. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama kisha ufanye mazoezi uliyopewa.
3. Rejelea maelezo ya sehemu ya **Kiangaza** katika ukurasa wa 54 unapofanya zoezi hili.
4. Zingatia vipengele vyote vya ushairi.
5. Soma diwani teule ya mashairi au utafiti diwani yoyote ya mashairi katika mtandao salama.

8. Kusoma kwa ufahamu

a. Kifungu cha simulizi
Jitathmini 8.1 (ukurasa wa 54-55)

1. Kusoma kifungu hutusaidia kupata ujumbe kuhusu suala fulani.
2. Maswali kuhusu matukio katika kifungu, eneo la matukio hayo, watendaji wa matukio hayo na matumizi ya lugha katika kifungu.
3. Matumizi ya lugha, mtiririko wa matukio, matendo ya wahusika.

Kifungu cha simulizi 1

4 (a).

i. Shule ya Msingi ya Jitahidi.

ii. Walipata ajali ya barabarani na kuaga dunia.

iii. Gredi ya Nane.

iv. Alihamia mjini.

(b). Chumba walichokuwa wamekodisha kilifungwa kwa kushindwa kulipa kodi.

(c) Fanya shughuli hii na mwenzako.

(d) Fanya utabiri unafungamana na kifungu kama vile, Petu alitia bidii masomoni na kufaulu.

(e).

Wavyele - mama na baba ya mtu (wazazi)

Kuaga dunia - kufariki

Kumwendea mrama - mambo kumwia mabaya au kumwendea kombo

Uvundo - harufu mbaya

Akagutuka - akashtuka

Hamamuni – chumba maalum cha kuogea.

5. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama kisha ufanye mazoezi uliyopewa.

Kifungu cha simulizi 2

Jitathmini 8.2 (ukurasa wa 55-56)

1.(a) Kutokana na uchafu.

(b) Ugonjwa wa kipindupindu

(c) Ili kuzuia ugonjwa na soko liweze kufunguliwa.

2. Fanya zoezi hili na mwenzako.

3. Soko lilifunguliwa, ugonjwa wa kipindupindu uliacha kuenea

4.

- Hughasi - huudhi au kukera
- Kusambaa - kuenea kila mahali
- Mwalimu wa zamu - mwalimu anayefuatilia shughuli za shule katika kipindi fulani
- Walijumuika - walijikusanya pamoja na watu wengine.

5. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama kisha ufanye mazoezi uliyopewa.

Kifungu cha simulizi 3

Jitathmini 8.3 (ukurasa wa 56)

1 (a) Kuusafisha Mto Sikite

(b) Ukulima, kunywesha mifugo, matumizi ya nyumbani

(c) Ili kuwasaidia wanakijiji.

(d) Hali ya kawaida ilirejea, mto uliwasaidia wanakijiji tena.

2.

piga gumzo – fanya mazungumzo yasiyo na lengo mahususi la kuzungumzia.

piga mbizi - ogelea

kitongoji - kijiji

biwi la taka - taka nyingi zilizotupwa mahali pamoja

3. d, e, b, c, a

4. Sentensi ziwe sahihi.

b. Kifungu cha ufahamu
Jitathmini 8.4 (ukurasa wa 56-57)

1. Matumizi ya lugha, maudhui ya kifungu, aina ya kifungu husika.

Kifungu cha ufahamu 1

Ubaguzi wa kijinsia

2 (a) Babake, kwa kuwa alikuwa mtoto wa kike

(b).

- Jinsia - suala linalohusu kuwa mwamamume au mwanamke
- Mume - jinsia ya kiume
- Jamii - watu wa kitovu kimoja
- Alihofia - alikuwa na woga
- Simanzi - huzuni
- Kuwaza – kufikiri hasa kuhusu njia ya kutatua matatizo

(c) Andika daftarini au kwenye shajara yako.

4. Fanya shughuli hii na mzazi au mlezi wako.

Kifungu cha ufahamu 2

Jitathmini 8.5 (ukurasa wa 57)

1 (a) Jinsia ya kike na kiume inapaswa kupewa nafasi sawa ya kujiendeleza kimaisha kupitia kwa elimu.

(b)

- Jinsia - suala linalohusu kuwa mwamamume au mwanamke.
- Anapobaleghe - anapofikisha umri wa kuweza kupata mtoto
- Kuozwa - kukabidhi binti katika ndoa
- Nadra – kwa uchache
- Wamepiga hatua – wamesonga mbele

2. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama kisha ufanye mazoezi uliyopewa.

Kifungu cha ufahamu 3

Jitathmini 8.6 (ukurasa wa 57)

1. Ili kupata ujumbe kuhusu suala fulani.

2 (a).

- Kuchukulia kuwa jinsia moja ni bora kuliko nyingine
- Kudunisha jinsia ya kike

(b) Watu hawana budi kuziacha mila potovu zinazomdhalilisha mtoto wa kike na kupigania kumpa nafasi sawa ya kielimu kama mtoto wa kiume.

3. Toa jibu na ueleze kwa nini unatoa jibu hilo.

4.

- Mila - mambo yanayofanywa na jamii fulani ambayo yanalingana na asili yao.
- Tamaduni - desturi ya kundi la jamii fulani.
- Kitega uchumi - kitu kinachoweza kuleta mapato.

5. Tunga sentensi sahihi.

c. Kifungu cha kushawishi

Jitathmini 8.6 (ukurasa wa 57-58)

Kifungu cha kushawishi 1

1. Kinatoa taarifa kwa nia ya kumfanya msomaji akubaliane na mtazamo wa kifungu hicho.
2. (a) Njia za mawasiliano zimebadilika kadri nyakati zinavobadilika. Zamani watu walituma ujumbe kwa kutumia nyenzo kama kupiga ngoma na kuwasha moto. Baada ya kupiga hatua ya kimaendeleo, waliwasiliana kwa njia ya barua.
   Katika nyakati hizi za maendeleo ya kidijitali, watu huwasiliana kwa vifaa vya kidijitali kama vile simu na kompyuta.
   (b) Tumia kamusi kufanya zoezi hili.
   (c) Maendeleo ya kiteknolojia yameleta mabadiliko mbalimbali hasa katika sekta ya mawasiliano.

4. Fanya zoezi hili na mzazi au mlezi wako.

Kifungu cha kushawishi 2

Jitathmini 8.8 (ukurasa wa 58)

1. Kwa kuzingatia ujumbe unaopitishwa, matumizi ya lugha, maelezo yanayovutia kuhusu suala linalotolewa ushawishi kulihusu.
2. (a) Msamiati wa biashara kama vile mnunuzi, bidhaa, muuzaji, malipo, pesa taslimu.
   (b)

- Mnunuzi – mteja, mtu anayenunua bidhaa fulani
- Bidhaa – vitu vinavyouzwa na kununuliwa
- Muuzaji – mtu anayeuza bidhaa fulani
- Malipo – pesa anazotoz mnunuzi kugharimia bidhaa fulani
- Pesa taslimu – sarafu au noti alizonazo mnunuzi za kugharimia bidhaa fulani.

(c) Mnunuzi anashawishiwa kuwa makini anaponunua bidhaa hasa mtandaoni. Kwanza anastahili kukagua bidhaa na kuridhishwa nayo kabla hajafanya malipo yoyote. Baada ya kulipa, anafaa kuhakikisha kuwa anapewa stakabadhi za ununuzi kama vile risiti kwani huo ni ushahidi wa manunuzi yake.

Kifungu cha kushawishi 3
Jitathmini 8.9 (ukurasa wa 58-59)

1. (a) Manufaa ya uvumbuzi wa vifaa vya kidijitali katika biashara. Kwanza, biashara imevuka mipaka ya mataifa na kuwa ya kimataifa kupitia vifaa vya kidijitali. Pia, usimamizi wa biashara umerahisishwa kwani mwenye biashara anaweza kufuatilia shughuli za uuzaji kutoka sehemu yoyote ya ulimwengu.

(b) Biashara, tarakilishi, uvumbuzi, hesabu, rekodi

2. Manufaa ya vifaa vya kidijitali katika kuendesha biashara. Muuzaji na mnunuzi wanashawishiwa kukumbatia matumizi ya vifaa vya kidijitali ili kupunguza gharama ya kwenda kununua au kuuza bidhaa dukani au sokoni.

d. Kifungu cha mjadala

Jitathmini 8.10 (ukurasa wa 59-60)

1. (a) Ili kupata ujumbe au taarifa zinazowasilishwa.

(b) Hakiki majibu yako kwa kuzingatia sehemu ya **Kumbuka** katika ukurasa wa 59.

(c) Kusoma kwa makini na kuelewa msamiati uliotumika.

(d) Kusoma kwa makini na kuelewa msamiati uliotumika.

2. (a) (i) Kitendo cha kutenga sehemu ya kipato kwa ajili ya matumizi ya baadaye.

(ii) mapema

(iii) Mtu yeyote anayetaka kuweka akiba

(iv) Hurahisisha kuweka akiba kwa kudhibiti mianya ya matumizi ya pesa.

(v) Haba nah aba hujaza kibaba.

(b) Kuanza mapema, kutenga pesa za kuweka akiba pindi mtu apatapo kipato, kuandika bajeti na kutenganisha akaunti.

(c) Kuwa na kipato kidogo, matumizi ya kiholela na ununuzi wa ghafla, kukosa bajeti na mfumuko wa bei.

3. (a) Fedha anazopata mtu kama malipo au faida za biashara

(b) Makadirio ya mapato na matumizi

(c) Anakohifadhi pesa mteja wa benki yoyote

(d) Matakwa au haja

(e) Kupanda kwa bei za bidhaa

4. Unaweza kuandika daftarini au kwenye kifaa cha kidijitali.

5. Kuweka akiba huweza kuwa rahisi kwa kuzingatia hoja zilizotolewa lakini pia huweza kuwa ngumu hoja hizo zisipozingatiwa.

6. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama kisha ufanye mazoezi uliyopewa.

7. Unaweza kumsomea kitabuni au kwenye mtandao salama kisha umweleze jinsi ya kupata habari mahususi.

4. **Kusoma kwa mapana**

Matini ya kujichagulia
Jitathmini 9.1 (ukurasa wa 60-61)
1. Taja matini unazopenda kuzisoma.
2. Hakiki majibu yako kwa kurejelea sehemu ya Kumbuka.
3. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama kisha ufanye mazoezi uliyopewa.
4. Nakili msamiati na maana yake. Hakikisha sentensi unazotunga ziko sahihi kisarufi.
5. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama kisha ufanye mazoezi uliyopewa.
6. (a) Umuhimu wa michezo ya riadha.
(b) Nakili msamiati mpya katika matini hiyo.
(c) Tumia msamiati huo kutunga sentensi.
(d) Fupisha kwa kuzingatia hoja muhimu pekee.
(e) Hakiki majibu yako kwa kurejelea sehemu ya **Kumbuka** katika ukurasa wa 61.

5. **Kusoma kwa ufasaha**

a. Kifungu cha nathari 1
Jitathmini 10.1 (ukurasa wa 61-62)
1 (a).

- Matamshi bora/sahihi ya maneno.
- Kasi inayofaa (si haraka sana wala si polepole mno).
- Kutumia sauti inayosikika na kiimbo/toni mwafaka.
- Kuzingatia alama za uakifishaji (vituo, koma, n.k.).
- Kutumia ishara za mwili na viziada lugha vifaavyo.

(b) Kunamwezesha msikilizaji kupata ujumbe uliokusudiwa.
2 (a) Yanahusu kutamka sauti na maneno ya lugha husika (Kiswahili) kwa usahihi na ipasavyo bila kuyakata, kuyakopesha, au kusita sana.

(b) Makala yote ya nathari au maandishi yoyote ya kielimu, habari, matukio, na mawazo yanayohitaji kueleweka kwa urahisi na wasikilizaji.
4. Ni wajibu wetu kuyatunza maliasili yetu kwani matumizi yafaayo ya maliasili hayo huleta maendeleo katika jamii na taifa.
6. Hakiki hoja zako kwa kurejelea sehemu ya **Kumbuka** katika ukurasa wa 62.
7. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama kisha ufanye mazoezi uliyopewa.
8. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama kisha ufanye mazoezi uliyopewa.
9. Fanya zoezi hili na mzazi au mlezi wako.

b. Kifungu cha nathari 2

Jitathmini 10.2 (ukurasa wa 62-63)

1 (a) Matamshi bora, kasi ifaayo, ishara zifaazo, kiimbo mwafaka, kiwango kinachofaa cha sauti.

2. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama kisha ufanye mazoezi uliyopewa.
3. Tafiti makala katika vitabu vya marejeleo au katika mtandao salama.
4. Fanya zoezi hili na mzazi au mlezi wako.

6. **Ufupisho**

Jitathmini 11.1 (ukurasa wa 63)

1. Ufupisho ni uandishi au uelezaji wa habari muhimu kutoka katika kifungu kirefu cha matini (kama vile hadithi, makala, hotuba au taarifa) kwa kutumia maneno machache na kwa ufupi, lakini bila kupoteza maana ya kimsingi, muktadha, au ujumbe mkuu uliokusudiwa na mwandishi wa awali.

2

- Kusoma kifungu kwa makini na kwa kurudia ili kukielewa vyema.
- Kutambua na kuorodhesha mawazo makuu na hoja zote za kimsingi.

- Kuondoa maelezo yasiyo ya lazima, kama vile: vivumishi, vielezi, mifano, marudio, pambo la lugha na sifa za ziada.
- Kutumia lugha fupi, fasaha, na sahihi kulingana na kanuni za sarufi.
- Kuhakikisha kuwa maana ya awali na mtiririko wa kimantiki wa taarifa haupotei wala kubadilika.
- Kupanga maelezo kwa mpangilio sahihi unaoendana na matini ya asili.

3.

- Huokoa muda wa msomaji au msikilizaji kwa kumwezesha kupata ujumbe kiini kwa haraka.
- Husaidia kubaini na kushika mawazo makuu kwa urahisi bila kutatizwa na habari nyingi za pembeni.
- Hurahisisha uhifadhi na ukumbukaji wa kumbukumbu muhimu.

4. (a) Tatizo kuu lililokuwepo katika kijiji cha Umoja lilikuwa ni uhaba mkubwa wa maji safi. Hali hii iliwalazimu wanakijiji kutembea umbali mrefu ili kutafuta na kuchota maji kutoka mtoni, jambo ambalo lilisababisha watoto kuchelewa shuleni na watu wazima kupoteza muda mwingi wa kufanya kazi za uzalishaji.

(b) Baada ya serikali ya kijiji kuona mateso na changamoto hiyo, ilichukua hatua ya kuamua kuchimba kisima kikubwa karibu na makazi ya watu. Mradi huo ulifanikishwa kupitia ushirikiano wa karibu na wa pamoja kati ya viongozi wa kijiji na wananchi wenyewe.

(c)

- Changamoto ya uhaba wa maji safi katika kijiji cha Umoja na athari zake kwa maisha ya kila siku.
- Uamuzi na hatua ya serikali ya kijiji ya kuchimba kisima karibu na makazi.
- Ushirikiano thabiti kati ya viongozi na wananchi katika kutekeleza mradi wa maji.
- Kukamilika kwa kisima, upatikanaji wa maji kwa urahisi, na uboreshaji wa maisha ya wanakijiji.

(d) Mfano wa ufupisho:
Kijiji cha Umoja kilikabiliwa na uhaba wa maji safi uliosababisha watoto kuchelewa shuleni na watu kupoteza muda wa kazi wakiyatafuta mtoni. Ili kutatua changamoto hii, serikali ya kijiji kwa ushirikiano na wananchi walichimba kisima kikubwa karibu na makazi yao. Kisima hicho kilipokamilika, maji safi yalipatikana kwa urahisi na kuboresha maisha ya wanakijiji yaliyokuwa magumu hapo awali.

(e)

- Katika mawasiliano ya kila siku, ufupisho hutuwezesha kufikisha ujumbe kwa haraka na kwa usahihi bila kupoteza muda.

- Husaidia kuepuka mkanganyiko kwa kuondoa maneno mengi yanayoweza kupotosha kiini cha ujumbe.

5. Ufupisho ni kuandika habari muhimu kutoka katika kifungu kirefu kwa maneno machache bila kupoteza maana ya msingi.

6. Fanya zoezi hili na wenzako.

7. Soma vitabu vya marejeleo au usakure katika mtandao salama kupata kifungu kuhusu maadili. Soma kifungu hicho kisha ufanye mazoezi uliyopewa.

8. Mweleze mzazi au mlezi wako kuwa ufupisho unajumuisha hatua tatu kuu:

- Kusoma na kuelewa: Kusoma matini kwa makini ili kupata picha kamili ya ujumbe.
- Kuchuja na kuchagua: Kutenga mawazo makuu na kutupa kando maelezo yasiyo ya lazima.
- Kuandika upya: Kuunganisha mawazo makuu kwa kutumia lugha fupi, fasaha, na yenye mtiririko sahihi bila kubadilisha ukweli au maana ya mwandishi wa asili.